IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI

N02/251/H(1)T

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Monday 4 November 2002 (morning)
Lundi 4 novembre 2002 (matin)
Lunes 4 de noviembre de 2002 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1 (Text handling).
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir ce livret avant d’y être autorisé.
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l’épreuve 1 (Lecture interactive).
- Répondre à toutes les questions dans le livret de questions et réponses.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos requeridos para la Prueba 1 (Manejo y comprensión de textos).
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

# Ebbo awika na 'Mi Mmasai'

Na Joe Rugarabamu

❶ Kila aliyesikia wimbo mpya wa Bwana Abel Loshilaa Motika au kwa kifupi Ebbo, unaoitwa Mi Mmasai ameguswa na umahiri wa msanii huyu chipukizi kwa mambo mengi. Katika miondoko ya hip hop ambayo ndiwo inawika katika muziki wa kizazi kipya, wameanza kujitokeza wasanii wanaotumia akili sana na ujuzi wa hali ya juu kiasi cha kuwavutia watu wa rika mbalimbali tofauti na hapo mwanzoni.

❷ *Academia* kama kawaida yake ya kutetea maslahi na vipaji vya vijana ilifanya juhudi kubwa kumpata na kuongea na kijana Ebbo ili kufahamu hisia zake na mantiki ya wimbo huu ambao ghafla umechukua namba moja katika chati za redio karibu zote hapa nchini. Ebbo ni kijana mwenye uelew wa hali ya juu wa mambo ya ulimwengu na ukiongea naye unavutiwa na upeo wake wa juu katika fani ya muziki na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

❸ Amekuwa akitunga nyimbo mbalimbali kwa takribani miaka kumi lakini kama kujifurahisha (hobby) zaidi na si kibiashara. Baada ya kugundua kuwa kipaji chake kina thamani kibiashara, ameanza kwa kutunga nyimbo nane anazorekodi sasa hivi katika albamu yake ya kwanza iitwayo "Fahari yako".

❹ Ebbo kama walivyo Wamasai wote anajivunia mila na utamaduni wake kiasi cha kutia moyo hasa kipindi hiki ambapo kizazi kipya kiko katika njia panda kusahau utamaduni wetu na kuhusudu kila kitu cha kigeni. Anao msimamo mkali kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kuenzi tamaduni za kiafrika.

❺ Anasema Mmasai ametunza hadhi yake kwa kujitambua utu na thamani yake kuliko makabila mengine hapa nchini. Hisia zake anazoziimba kimasai katika wimbo wake na hata nyimbo nyingine katika albamu yake anayoiandaa zinadhihirisha fahari ya kujitambua kwa Mmasai na ujumbe wake kwa jamii ni kuwa utu wa mtu unadumishwa kwa kujitambua na kujithamini.

❻ Ebbo anasema Mmasai anapolazimika kuondoka katika mazingira yake ya ufugaji na kwenda mjini anakumbana na matatizo mbalimbali pamoja na kutaniwa na kuonekana hajaendelea. Hayo matatizo hayamyumbishi Mmasai kwani amekubali utamaduni wake na anapenda kuonekana halisi. Ndiyo maana anajivuna na kusema "Naruhusu kushangaa kwa wanyeji na wageni;" maana yake watanzania na watalii.

❼ Katika nyanja za utalii Ebbo anasisitiza kuwa kuendeleza mila za Kimasai kumeliingizia taifa letu fedha nyingi za kigeni kupitia kwenye utalii kiasi kwamba kila mtalii hupenda angalau aongee na Mmasai, apige picha na Mmasai au hata afike katika makazi ya kimasai ajionee wanaishije.

❽ Ebbo ametunga nyimbo nyingine katika albamu ambayo inaelekea itakuwa ya hali ya juu sana ikitoka. Nyimbo zilizoko katika Albamu yake ya Fahari yako ni Mi – Mmsai, Nini fahari yako, Maneno mbofumbofu. Sitaki tena pombe, Vipi hatuoni mwanga, Muwe na huruma, Nani huyo na Mi Mmasai (Remix). Akielezea kila wimbo na kukuimbia kidogo unatamani asiache na unagundua kuwa zote zina ujumbe mzito na ametumia akili ya hali y juu kuzitayarisha.

ACADEMIA (April 2002)

**KIFUNGU B**

# Mama Terry

ajibu maswali yenu

1 **Mama Terry kama ndugu Samson E. alivyoelezea, katika academia tolea 009 kuwa wewe ni uona wetu na mama yetu pia, napenda kujua ni nini hasa kinachowafanya vijana wetu wengi kujihusisha na madawa ya kulevya, ili hali wataalamu wa magonjwa ya akili wanasema kuwa karibu 80% ya vichaa inatokana na hayo madawa? Je kufanyike nini ili kulinusuru hili kundi?**

*Japhet Alexander Tabata, Dar es Salaam.*

2 Mpendwa Japhet, ili kuweza suala la madawa ya kulevya na vijana inampasa mtu kwanza kulielewa suala zima la vijana na ujana, na hii itaingiza ndani suala la maumbile ya mwanadamu. Mwanadamu ameumbwa kwa namna ambayo anavyo vipindi vitatu muhimu katika maisha yake. Kipindi cha kwanza ni utoto ambapo tunaona kuwa mtoto anataka kujifunza kila kitu na ni wakati wake wa kuanza kuweka mambo kutegemeana na mazingira ambayo mtoto huyu atakuwa analelewa. Iwapo kama mtoto huyu katika kipindi hiki atapata mazingira mazuri ambayo yana msingi bora na uongozi thabiti wenye maadili mema, basi mtoto huyu atakuwa katika misingi hiyo katika umri wake huo na hata wakati mwingine anaweza kuiendeleza misingi hiyo katika maisha yake ya baadae.

3 Kipindi cha pili ni kipindi cha ujana. Hiki ndicho kipindi kigumu katika vipindi vyote katika maisha ya mwanadamu. Kwa lugha ya kigeni kipindi hiki huitwa "foolish age". Hapa kijana hutaka kuamini kuwa amekua na anajua. Tena anajua karibu kila kitu na mara nyingi sana hujaribu kujipa uhuru usio na mipaka. Hiki ni kipindi ambacho kijana hupenda kuyaiga yale yote ambayo hudhani kwamba yanampa starehe na burudani ya aina fulani, kimwili, kiakili na kihisia.

4 Hiki ni kipindi muafaka kabisa cha kijana kuweza ama kuwa na maadili mema iwapo atapata uongozi mzuri wa kuweza kumsisitizia hayo, ama kuwa na mmomonyoko wa maadili na kuishia kupotoka kabisa. Mara nyingi sana katika kipindi hiki cha ujana, kijana hutumia zaidi hisia na akili zake bila kuongozea busara.

5 Kipindi cha tatu ni cha utu uzima na uzee. Hapa mtu huishi zaidi kwa kuzingatia mafundisho aliyoyapata katika maisha yake, "experience" na hivyo basi hutumia zaidi akili na busara kuliko hisia na akili.

6 Lakini leo tunauzungumzia ujana. Kipindi hiki cha "foolish age", kipindi ambacho mtu huona kuwa amekua na anayajua mengi a hawezi kuelezwa kitu. Kipindi hiki Japhet, ni cha hatari sana.

7 Sasa tuyaangalie madawa ya kulevya. Kwa kipindi kirefu sasa hapa ilimwenguni biashara ya madawa ya kulevya imekuwa ikishamiri sana. Neno lenyewe biashara tayari linakueleza mengi. Ndio, madawaya kulevya hutumika kama biashara tena biashara kubwa na yenye kuleta fedha nyingi sana. Watu mbalimbali na hata mataifa yaani baadhi ya nchi duniani hujihusisha na biashara hii.

8 Madhara makubwa zaidi yanayotokana na utumiaji wa madawa ya kulevya, ni ile hali tegemezi inayojitokeza kwa utumiaji yaani anapata uzoefu na mwili wake unakuwa unahitaji matumizi haya mara kwa mara.

9 Sasa basi kwa kuwa vijana wanao umri mkubwa zaidi wa kuishi kuliko watu wazima na wazee, na kwa vile hii ni biashara yenye kuleta kipato kikubwa kwa wale wanaoifanya, kundi hili la vijana ndilo linalengwa zaidi katika matumizo hayo. Hii ni kwa kuwa vijana wakianza kutumia basi watatumia kwa kipindi cha muda mrefu zaidi. Ni rahisi zaidi kwa kijana kushawishika kutumia madawa hayo kuliko rika lingine lolote kwani kama nilivyosema kipindi cha ujana ni rahisi zaidi kupotoka.

10 Nija za kutumia ili kuweza kulinusuru hili kundi, kwanza ni kuandaa mazingira yaliyo na maadili mema ndani ya jamii yenyewe, katika suala zima la malezi ya watoto na vijana. Yawepo maadili bora kwa manufaa ya kuwajenga kimaadili hasa mienendo ya na tabia zao.

11 Wazazi vile vile wawe na muda mrefu zaidi wa kukaa na watoto na vijana wao na waweze kuwa wazi zaidi katika mafundisho yao Viongozi wa dini waelewe kuwa misingi bora yapaswa ifundishwe kwa waumini wao tangia wakiwa watoto na hasa kwa vijana.

12 Serikali nayo iweke misingi ama mazingira bora kwa vijana na sio kuwaacha solemba mara wanapomaliza masomo yao ya shule za msingi ama sekondari kama ilivyo sasa. Vijana wanapaswa kuwekewa mazingira ambayo yanawapa matumaini ya wao kuwa na maisha bora baadae.

ACADEMIA (January 2002)

**KIFUNGU C**

*Soma shairi lifuatalo na kisha jibu maswali yanayofuata*

**WASIA**

Adabu kitu adhimu, kwa fakiri na tajiri,
Ni pambo kwa wanadamu, wakubwa na asighari,
Tena hujenga nidhamu, raia na askari,
Tutakuwa mahashumu, haya tukizingatia.

Ingawa ni jambo gumu, kutii pasi hiari,
Kwanza mtii Rahimu, mitume na maamiri,
Wazazi nao walimu, na wakubwa usihuri,
Tutakuwa mahashumu, haya tukizingatia.

Ukweli unalazimu, pale ilipo dosari,
Ingawa ni mbaya sumu, usipotoshe habari,
Uwongo usiazimu, na kujitia kiburi,
Tutakuwa mahashumu, haya tukizingatia.

Kisha hili ufahamu, subira huvuta heri,
Mambo yakiwa magumu ni bora ukasubiri,
Utakuja jilaumu kutaka mambo kwa mori,
Tutakuwa mahashumu, haya tukizingatia.

Haifai wanadamu, kupenda mambo ya shari,
Hasa yanayodhulumu, kwa kukaka utajiri,
Adili yatuhukumu, huo sio uhodari,
Tutakuwa mahashumu, haya tukizingatia.

Vazi la kujiheshimu, nadhifu na mashuhuri,
Hata ndani ukidumu, au unaposafiri,
Vaa nguo maalumu, zile zinazositiri,
Tutakuwa mahashumu, haya tukizingatia.

Uitafute elimu, ya mila na desturi,
Isambae kwenye damu, huku ukitafakari,
Mwenye pupa hali tamu, wamenena wahubiri,
Tutakuwa Mahashumu, haya tukizingatia.

Hapa ndio tahatimu, imegota misitari,
Ningependa ufahamu, uvivu una hatari,
Usilaze yako damu, jitume ongeza ari,
Tutakuwa mahashumu, haya tukizingatia.

Robert S Mfilinge, DAR LEO (June 2000)

**KIFUNGU D**

# Rubani mwanamke Kenya asimulia masahibu ya angani

1 Akiwa na furaha ya kupata leseni ya urubani, mwanamke, Cathleen Kang'ethe, alichukua ndege ndogo aina ya Cessina uwanja wa ndege wa chuo cha Wilson jijini Nairobi kuelekea kwenye mbuga ya watalii ya Maasai Mara.

2 Ilikuwa alasiri tulivu ambayo haikumpa mashaka yoyote yeye na mwanafunzi mwenzake waliyeongozana naye kwenye ndege hiyo inayobeba watu wawili.

3 "Namna ya kutua ndiyo kitu nilichokiwaza kwanza," anaeleza Cathleen wakati alipozungumza na gazeti la *National* hivi karibuni.

4 Kutua kwenye kiwanja cha mbuga hiyo, mara nyingi huwa ni mtihani mkubwa kwa marubani wanafunzi. Mbele ya uwanja huo kuna vilima viwili ambapo rubani lazima apenye katikati yake ili atue.

5 "Kama wewe ni mgeni katika eneo hilo, unaweza kujikuta umetoka kwenye njia yako bila kujua. Mimi nilijua nitaifikia njia yangu ya kutua baada ya kutembea kilomita fulani," anaeleza na kuongeza: "Baada ya kutembea mwendo huo nilianza kushusha ndege taratibu."

6 "Hapa ndiyo kasheshe ilianza Ndege ilianza kuyumba na kutoka kwenye njia. Tuliona kifo kimetuzunguka sasa," anasema.

7 Anasema, ingawa lengo alitaka ashuke taratibu, ndege yake ilishuka kwa kasi. "Kwa dakika chache tulikuwa tumeshuka maelfu ya kilomita," anaeleza.

8 Darasani tulikuwa tumefundishwa njia nyingi za kukabiliana na matatizo kama hayo, lakini ilikuwa mara yangu ya kwanza kuyatafsiri kwa vitendo mafunzo hayo.

9 "Ingawa nilikuwa nikirusha ndege kwa mwaka mzima tuliokuwa masomoni, hali hii ilinishtua sana. Nilikuwa nashuka kwa kasi ya kutisha. Kifaa cha kuonyesha hali ya ndege hakikuonyesha hitilafu yoyote. Injini, mafuta na bodi ya ndege vilikuwa sawasawa," anasema.

10 Cathleen anasema, baada ya kuona ndege yake iko sawasawa, alipunguza kasi ya injini ili kuangalia kama itapunguza mwendo, lakini haikuwa hivyo.

11 "Nilipomtazama usoni mwenzangu niliona kwamba alikuwa na hofu kubwa. Mimi nilijikaza na kuendelea na harakati zangu za kujaribu kutatua tatizo hilo," anasema na kuongeza: "Ghafla niliona ndege inaelekea kwenye kilima. Nilichanganyikiwa lakini baadaye nilitulia kufikiria haraka."

12 Cathleen anasema: "Nilisikia kama sauti toka mbinguni ikielekeza pinda kulia… pinda kulia. Nilipofanya hivyo katikati ya vilima viwili na kisha nikaanza kuuona uwanja. Nilikwenda hadi chini na kutua salama salamini."

Oscar Mbuza, MAJIRA (April 2002)